

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKUU WA MKOA WA NJOMBE

SIMU: 026- 2790001

FAX: 026- 2790001



OFISI YA MKUU WA WILAYA,

S.L.P 02,

LUDEWA.

**TAARIFA KWA UMMA**

Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Mhe. Andrea Tsere leo Juni 05, 2022 ameungana na wananchi wa Wilaya ya Ludewa katika kuadhimisha siku ya Mazingira Duniani.

Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika Makao Makuu ya Wilaya ya Ludewa kwenye viwanja vya sokoni Mkuu wa Wilaya amewahutubia wananchi na kuwasisitiza kuvitunza vyanzo vya maji na amewataka wananchi wote kuongeza juhudi za upandaji miti ili kuondokana na ukame usio walazima.

Aidha Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa Andrea Tsere amewaagiza viongozi wote wa Vijiji kwenye Wilaya ya Ludewa kusimamia sheria na taratibu za upataji vibali vya uchomaji moto ili kuondokana na uharibifu mkubwa unaotokana na uchomaji moto bila kibari.

Katika mkutano huo wamehudhulia viongozi mbalimbali wakiwemo wakuu wa idara wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa aliye wakilishwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Bw. Gilbert Ngailo.

Pamoja na mambo mengine Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ludewa ametoa elimu ya Sensa ya Watu na Makazi na akaongeza kwa kusema kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ameifanya Tanzania kuwa ni nchi yenye watalii wengi amewaomba wananchi kuitazama filamu ya The Royal Tour inayo oneshwa leo kwenye wilaya hiyo yenye lengo ya kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini

**Chrispin B.Kalinga**  
**Afisa Habari (W) Ludewa**